

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI

18 MEI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI – TAREHE 18 MEI, 2018

I. DUA:

II. TAARIFA YA SPIKA:

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

IV. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**266. MHESHIMIWA KHADIJA NASSIR ALI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Miongoni mwa matakwa ya Serikali ni
kuwawezesha Vijana na Wanawake kiuchumi:-

Je, Serikali inatekelezaje suala hilo.

267. MHESHIMIWA ZAINAB ATHUMAN KATIMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Vijana wengi wanakosa sifa za kuajiriwa kwa kukosa uzoefu kazini:-

Je, Serikali haioni haja ya kutungwa kwa Sera ya mafunzo kwa vitendo kazini kwa wahitimu wa Elimu ya Juu na Vyuo vya Ufundi (*Internship Policy for Higher Learning Institutions and Technical Colleges Graduates*) ili Vijana waweze kupata ujuzi utakaoendana na mahitaji ya soko la ajira.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

268. MHESHIMIWA RAPHAEL JAPHARY MICHAEL (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mhe. Rais katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, aliahidi kujenga km10 za barabara ya lami katika Manispaa ya Moshi:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo;
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kusaidia Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kujenga mitaro katika barabara zake za lami ili kuzifanya zidumu muda mrefu.

269. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imeanzisha Tume ya Huduma kwa Walimu (TSC) kwa lengo la kutatua matatizo ya Walimu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha Tume hiyo ili ifanye kazi kikamilifu kama ilivyokusudiwa.



OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

270. MHESHIMIWA PROSPER JOSEPH MBENA (MOROGORO KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Nchi nyingi duniani ikiwemo Japan, Uholanzi na Marekani hutumia Wataalam wastaafu kwenye

sekta mbalimbali za uchumi katika shughuli mbalimbali za kutoa ushauri ndani na nje ya nchi zao; Wataalam hao (*Volunteers*) wanatoa mchango mkubwa kwenye kushauri:-

(a) Je, ni lini nchi yetu itaiga utaratibu huo mzuri wa kuwatumia Wataalam wake wastaafu ipasavyo badala ya kuwaacha tu mitaani;

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka kumbukumbu ya taarifa ya Wataalam wastaafu wake (*directory*) kwa kila mmoja kwenye fani yake (*profession*) ili kuweza kuwatumia Wataalam wastaafu hao pale ushauri wao utakapohitajika.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

271. MHESHIMIWA OTHMAN OMAR HAJI (GANDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kuwa na uchakavu wa mitambo ya kuongozea ndege na miundombinu duni ya usafiri wa Anga nchini, TCAA imechaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Shirika la Usafiri wa Anga Duniani kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 na hivyo kuwa

mwakilishi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC):-

Je, kupitia nafasi hii ya kipekee, Serikali kupitia TCAA ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya usafiri wa Anga hapa nchini ili iweze kulingana na ile ya nchi nyingine za SADC.

272. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Wakati akihutubia Mkutano wa Kampeni Kharumwa Mhe. Rais aliwaahidi Wananchi wa Nyang’hwale kwamba barabara ya Kahama – Busangi – Kharumwa – Buyagu – Busisi itajengwa kwa kiwango cha lami; na Ilani ya CCM 2015 – 2020 imesema barabara ya Kahama – Buhige – Solwa – Mwanangwa itafanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami:-

Je, kuna maandalizi gani yanayoendelea ya kutekeleza ahadi hiyo ya Mhe. Rais na ile ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

273. MHESHIMIWA LATHIFA HASSAN CHANDE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Kiwanda cha kubangua Korosho cha Mtama *Cashewnut Factory* kilichopo katika Jimbo la Mtama kilikuwa chini ya Bodi ya Korosho na kiliuzwa kinyemela kwa Kampuni ya Lindi *Farmers* ambayo ilikodishwa kwa Kampuni ya Kichina ya *Sunshine Industrial Company Limited*, Kampuni ambayo inawalipa Wafanyakazi ujira wa shilingi 70 – 80 kwa kubangua kilo moja ya Korosho:-

- (a) Je, Serikali ina taarifa ya kukodishwa Kiwanda hicho;
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani juu ya mazingira magumu ya Wafanyakazi ambao hawana mikataba ya kazi katika Kiwanda hicho kinachomilikiwa na Wageni.

**274. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB
(B.L.W.):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Pamoja na kuwepo Viwanda vingi vya Sukari hapa nchini bado kumekuwa na uhaba mkubwa wa bidhaa hiyo hususan kwa upande wa Tanzania Bara; Mfano bei ya mfuko wa kilo 50 ni Shilingi 65,000/= kwa upande wa Zanzibar ambako kuna Kiwanda kimoja tu cha Sukari, lakini kwa Tanzania Bara mfuko huo wa kilo 50 huuzwa shilingi 120,000/=-

- (a) Je, kuna tatizo gani linalofanya Sukari iiuzwe bei ya juu kiasi hicho kwa upande wa Tanzania Bara;
- (b) Je, Serikali itachukua hatua gani ili kuweza kuwapatia Wananchi unafuu katika upatikanaji wa bidhaa hiyo;
- (c) Kwa upande wa Zanzibar katika kipindi ambacho matumizi ya Sukari kwa Wananchi yanaongezeka mfano, mwezi wa Ramadhani, Serikali inashusha ushuru wa kuingiza Sukari nchini; Je, kwa nini Serikali ya Muungano isizingatie utaratibu huu mzuri ili kuleta unafuu kwa Tanzania Bara.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

275. MHESHIMIWA RICHARD PHILIP MBOGO (NSIMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Tehama imekuwa kichocheo cha maendeleo na hivyo kurahisisha ulipaji wa gharama (*bills*) mbalimbali kupitia miamala kwa njia ya simu. Mathalan, muda wa maongezi, ving'amuzi, umeme, kodi na laini mbalimbali:-

Je, mlipaji aweke ushahidi wa aina gani katika kumbukumbu ngumu (*hard paper*) ili Wakaguzi

- wa TRA waone au TRA itaridhika
- kwa kumbukumbu ya muamala.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

276. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Wadhibiti Ubora wa Elimu ngazi ya Wilaya wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uhaba wa vitendea kazi:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kushughulikia changamoto za Ofisi hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yao;
- (b) Je, ni lini Wizara itapeleka Wadhibiti Ubora wa Elimu katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba badala ya kutegemea wale wa Halmashauri ya Mtwara.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
18 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**